TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

KONGAMANO LA KIMATAIFA KUHUSU PROGRAMU ZA KUNUSURU MAKUNDI YALIYOATHIRIKA ZAIDI NA UMASKINI, 14-18 JUNI 2010, ARUSHA TANZANIA

Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) imeandaa Kongamano la Kimataifa kuhusu Programu za Kunusuru Makundi yaliyoathirika zaidi na Umaskini. Kongamano litatoa fursa kwa watendaji wanaojihusisha na programu hizi kubadilishana uzoefu wa kuandaa na kutekeleza programu za aina hii. Benki ya Dunia huandaa makongamano ya aina hii kwa lengo la kutoa fursa ya kujifunza kuhusiana na programu za aina hii.

Uzinduzi wa Kongamano utafanywa na Kiongozi wa ngazi ya juu wa Serikali. Viongozi wengine waandamizi wa Serikali wanaotarajiwa kushiriki kwenye uzinduzi ni pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Utawala Bora) na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Ikulu. Kwa upande wa Benki ya Dunia watendaji waandamizi watakao shiriki kwenye ufunguzi ni pamoja na Mkurugenzi wa Benki ya Dunia hapa nchini Bwana John Murray McIntire. Kongamano litafanyika kwa muda wa siku tano kuanzia Jumatatu, Juni 14, 2010 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) na litaendeshwa kwa lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kihispania.

Wajumbe zaidi ya 200 kutoka nchi 42 duniani wanatarajiwa kuhudhuria; wajumbe ni pamoja na watendaji katika masuala ya fedha, uchumi, sekta za kijamii, miundombinu na kadhalika ambao watatoka serikalini, mashika ya wahisani, Benki ya Dunia, taasisi za kiraia, taasisi za elimu na mafunzo na sekta kibiashara. Kongamano limelenga mataifa yanayoendelea ambako programu za aina hii zinatekelezwa au zinatarajiwa kuanzishwa.

Kongamano litajihusisha zaidi na masuala yaa kuandaa programu hizi katika mazingira ya nchi zinazoendelea. Madhumuni ya Kongamano ni:

1. Kubadilishana uzoefu unajitokeza miongoni mwa wataalam, watendaji na wahusika toka nchi mbalimbali na wale wa Benki ya Dunia.
2. Kuweka msingi wa kuwa na jamii ya watendaji ambao wataendelea kubadilishana utaalamu katika mazingira ya nchi zinazoendelea.
3. Kuamsha ari ya kuelewa zaidi nafasi ya programu za kunusuru kama moja ya programu za kitaifa za kuhifadhi jamii maskini.

Kongamano litajumuisha vikao vya wajumbe wote, vikao katika vikundi vidogo na kutembelea miradi 10 ya jamii inayofadhiliwa na TASAF katika Halmashauri za Wilaya za Meru, Monduli na Longido katika Mkoa wa Arusha. Wajumbe watatembelea miradi ili kuwezesha kujifunza kutokana na mafanikio ya TASAF kwenye utekelezaji wa programu za aina hii na pia kuwawezesha washiriki kujenga uelewa kwa kushuhudia na kuona utekelezaji halisi na pia kubadilishana uzoefu kwenye maeneo ya miradi

husika. Kongamano litawezesha kupata taarifa na maelezo toka programu za nchi mbalimbali ambazo zitawekwa kwenye kitini cha miradi ya miradi ya kunusuru makundi haya maalum. Kitini kitatumika na Benki ya Dunia na mataifa mbalimbali kwa ajili ya mafunzo na kupashana habari kuhusu uandaaji na utekelezaji wa programu hizi.

Jamii maskini zinakabiliwa na mazingira hatarishi ambayo yanafanya iwe vigumu kutoka katika hali ya umaskini kwa urahisi. Programu za kunusuru makundi yaliyoathirika zaidi na umaskini na programu za uhawilishaji fedha kwa kaya maskini huwezesha kuinua hali na kuboresha maisha ya makundi haya kwa kuwapatia walengwa fedha mikononi mwao. Programu za kunusuru makundi maalum ndizo programu zinazoongoza na kutumika zaidi katika nchi zinazoendelea. Programu hizi huwezesha jamii na makundi husika kupata ajira ya muda na fedha ambazo hutolewa kama ujira wakati wa utekelezaji wa miradi ambayo kwa kiasi kikubwa uhusiana na miundombinu, hususan barabara na miundombinu ya umwagiliaji.

Katika Tanzania, Programu ya Serikali, TASAF kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia, kwa kipindi cha miaka 10 imewezesha jamii kutekeleza miradi ya aina mbalimbali katika wilaya zote za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Hadi sasa TASAF imewezesha jamii kutekeleza zaidi ya miradi 11,375 yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 197. Programu ya kunusuru makundi maalum ni moja kati ya njia ambazo Serikali inazitumia katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) kuyapatia makundi husika fedha hususan kaya zinazokabiliwa na uhaba wa chakula. Walengwa hupokea fedha kama ujira na pia hupata weledi. Hadi sasa TASAF imefadhili utekelezaji wa jumla ya miradi 928 ya aina hii na kuwezesha jamii na makundi maskini kupata jumla ya siku za ajira zaidi ya milioni 15 kwa kuwafikia walengwa zaidi ya 217,315 ambao wamepata fedha zaidi ya shilingi bilioni12.

Kongamano litahusika zaidi na mbinu na njia za uandaaji na utekelezaji wa programu za aina hii. Msisitizo mkubwa utakuwa kwenye kubadilishana taarifa na kujifunza kuptia uzoefu wa nchi mbalimbali na pia kupata taarifa muhimu. Kongamano litatoa fursa kwa nchi mbalimbali kuonyesha programu zinazotekelezwa katika nchi zao.

Zaidi ya mada 17 zitakazowasilishwa na kujadiliwa na wajumbe wa Kongamano; na zitahusu, pamoja na mambo mengine maeneo yafuatayo:

- Aina mbalimbali za programu za aina hii katika nchi mbalimbali na njia kuandaa programu mbadala.
- Mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa kundaa programu hizi, kama vile kiwango cha ujira, malipo, aina ya miradi, njia za kupata walengwa na kufanya uhakiki.
- Masuala ya kitaasisi na mgawanyo wa majukumu ngazi ya taifa, halmashauri na jamii.
- Masuala ya mazingira, jinsia na mawasiliano.
- Ufuatiliaji na usimamizi, mtiririko wa fedha, manunuzi, ushughulikiaji wa kasoro zinazoweza kujitokeza na uthibiti wa upotuvu na matumizi mabaya ya fedha..